
# KONDOO ALIYEPOTEA

## Darasa la 4
### la watoto

www.wingulamashahidi.org

by Denis & Devis Julius



# <u>**MADARASA YA WATOTO**</u>

Haya ni mafundisho maalumu kwa watoto wenye umri wa miaka 0-12. Ni madarasa mbalimbali ambayo wewe kama mzazi/ mlezi/ mwalimu yatakusaidia kumwongoza na kumwandaa mtoto katika ukuaji bora wa kiroho. Hili ni darasa la Tatu (4), Ikiwa hujapata miongozo ya nyuma basi utawasiliana nasi kwa namba zetu hizi, tuweze kukusaidia +255693036618/ +255789001312.

Bwana akubariki.

*Mithali 22:6 Mlee mtoto katika njia impasayo, Naye hataiacha, hata atakapokuwa mzee.*

~by Mchungaji Denis & Devis Julius.

**Darasa la Tatu (4)**

## KONDOO ALIYEPOTEA.

## UTANGULIZI:

Luka 15:3-7

Habari hii, ambayo Yesu aliiwasilisha kwa njia ya mfano wa mtu aliyekuwa na kondoo mia, kisha mmoja akapotea, akawaacha wale tisini na tisa na kwenda kumtafuta Yule mmoja aliyepotea, inafundisho kuu sana sio tu kwa watu wazima bali pia na kwa watoto. Kuielewa habari hii itawajengea kuijua sifa ya Yesu maishani mwao, jinsi anavyoweza kuwajali, hata pale wanapojiona wamepotea au wapweke. Vilevile kuwajengea moyo wa kuwafuatilia wengine waliopotea dhambini.

Fundisho hili ili walielewe vema. Wewe kama mwalimu utawapitisha katika hatua hizi sita (6).

1. Simulizi
2. Picha
3. Igizo
4. Fundisho
5. Nyimbo
6. Jaribio.

**SIMULIZI:**

Wewe kama mwalimu utaanza kwa kuwaeleza habari hiyo kwa lugha rahisi ya kiigizo yenye kueleweka kwao;

Kwa mfano: Kulikuwa na mchungaji mmoja ambaye alikuwa na kondoo mia, kila siku alikuwa akiwaangalia na kuwatunza, na kuhakikisha wana afya na furaha. Lakini ilitokea siku moja, kondoo mmoja kwenye machungo yao alienda  mbali na wenzake, hatimaye akapotea pasipo mchungaji wake kuwa na taarifa. Waliporudi nyumbani jioni baada ya safari ndefu, Yule mchungaji alipowahesabu ili kuangalia kama kondoo wake wote wapo salama, akagundua kuwa mmoja hayupo.

Angeweza kusema aah! Maadamu ni mmoja tu, mimi siwezi kurudi kule milimani mbali kumtafuta, lakini hakufanya hivyo, kwasababu aliwapenda kondoo wake wote, na wote walikuwa na thamani sawa machoni pake. Akawaacha wale tisini na tisa pale zizini wakiwa na chakula na maji, kisha akaanza safari yake ndefu ya kumtafuta kondoo wake mmoja aliyepotea.. Akawa anamwita! Huko na kule.. “Kondoo wangu uko wapi?”

Baada sana katika kuzunguka huko na huko ndipo akamwona, akiwa amenaswa katika bonde, akamtoa, akamweka mabegani mwake kwa furaha, na kumrudisha nyumbani, kisha akawaita marafiki zake na ndugu na kuwaambia nimempata kondoo wangu aliyekuwa amepotea.

*Mwisho*

Baada ya kuwasilimulia habari hiyo. Wasomee sasa katika biblia. Changua mtoto mmoja ajuaye kusoma kisha aisome kwa niaba ya wote.

(Wasisome kwenye simu. Tumia kitabu cha biblia).

*Luka 15:3 Akawaambia mfano huu, akisema,*

*4 Ni nani kwenu, mwenye kondoo mia, akipotewa na mmojawapo, asiyewaacha wale tisini na kenda nyikani, aende akamtafute yule aliyepotea hata amwone?*

*5 Naye akiisha kumwona, humweka mabegani pake akifurahi.*

*6 Na afikapo nyumbani kwake, huwaita rafiki zake na jirani zake, akawaambia, Furahini pamoja*

*nami, kwa kuwa nimekwisha kumpata kondoo wangu aliyepotea.*

*7 Nawaambia, Vivyo hivyo kutakuwa na furaha mbinguni kwa ajili ya mwenye dhambi mmoja*

*atubuye, kuliko kwa ajili ya wenye haki tisini na kenda ambao hawana haja ya kutubu.*

## **PICHA:**

Baada ya kuwahadithia habari, Tumia picha (Ikiwa unazo,) waweza kuprinti hizi zaweza wasaidia kuelewa vema habari hiyo;





## IGIZO:

Baada ya hapo, Tengeneza Igizo: Ikiwa una idadi ya watoto 3 na kuendelea, mmoja unamfanya mchungaji, wengine kondoo, na mwingine mmoja kama kondoo aliyepotea unampelekea mafichoni, kisha unawafundisha kumtafuta Yule aliyepotea.

Kuwafundisha kivitendo, huchangia pakubwa sana, habari hiyo kubaki kichwani kwa muda mrefu.

## FUNDISHO:

Baada ya hapo, waeleze sasa  maana ya hadithi hiyo;

Yesu anatufundisha nini?

- Anatufundisha upendo wake kwetu, pale tuwapo wapweke, yupo nasi wakati wote, na pale tujionapo tumepotea yupo tayari kutuokoa tena.
- Lakini pia Yesu anataka na sisi tuende kuwaleta wengine kwake waliopotea, mfano wa Yule mchungaji alivyofanya.

Kukariri:

Baada ya hapo, wafundishe kukariri, habari hiyo inatoka katika kitabu gani, na sura ya ngapi na mstari wa ngapi. (Luka 15:3-7)

Wafanyishe mazoezi hayo, mpaka kila mmoja aweze kuvitaja vifungu hivyo mwenyewe kutoka kichwani.

Kifungu cha kukariri kiwe hichi:

*Luka 15:7 Nawaambia, Vivyo hivyo kutakuwa na furaha mbinguni kwa ajili ya mwenye dhambi mmoja atubuye, kuliko kwa ajili ya wenye haki tisini na kenda ambao hawana haja ya kutubu.*

## **NYIMBO:**

Andaa nyimbo, au pambio, linaloendana na kupotea kwa kondoo, kisha wafundishe Kuimba:

Wafundishe Tenzi: Na. 30 – Nilikuwa kondoo aliyepotea..(Kama huijui tazama youtube). Au nyimbo nyingine uijuayo yenye maudhui hiyo hiyo ya Yesu kututafuta sisi na kutukomboa.

## **JARIBIO:**

Wakifuzu, madaraja yote hayo, sawa wape jaribio, kila mmoja katika wiki, aende kumuhubiria rafiki yake, kwa kuwaeleza hiyo hadithi na kwamba Yesu anampenda, na alikufa kwa ajili yake ili asipotee. Anamwita tena wokovuni.

Waje kukupa mrejesho, ni nani, na nani walienda kuwahubiria.

Rudia tena, kuwatuma kuwaeleza wengine na wengine.

Hilo litamsaidia na kumjengea mtoto njia ya kutumiwa na Bwana. Kumbuka kwa Bwana hakuna mtu mzima au mtoto, kwa njia hiyo hiyo

Mungu atamtumia kuwavuta wengine kwa Mungu. Hivyo darasa hilo lifanye kwa umakini, ukijua kuwa linazalisha askari wa ufalme.

## **Mwisho:**

Wawezeshe kuwasilisha walichojifunza mbele ya watu wengi, aidha kanisani, au mbele ya familia. Hiyo itawajengea ujasiri wa rohoni. Na pia itapima uelewa wao, ikiwa kuna mahali panahitaji matengenezo au La!.

Bwana akubariki.

Mawasiliano.

Huduma ya Nuru ya Upendo wa Kristo.
www.wingulamashahidi.org
+255789001312/ +255693036618
info@wingulamashahidi.org